**FOMU PLUPA L-2** **(r.10)**

# JAMHURI YA KENYA
## SHERIA YA MPANGO WA MIJI NA MATUMIZI YA ARDHI
## (*Nambari* 13 *ya* 2019)

## ILALNI KUHUSU KUKAMILISHWA KWA MPANGO WA USTAWISHAJI

Kichwa cha Mpango wa Ustawishaji: **Kurasimishwa kwa eneo palipotengewa utekelezaji wa Mpango wa Ujenzi wa Nyumba za Gharama Nafuu, Emgwe, Kaunti ya Nandi**

**Nambari ya PDP NRB/126/2025/01**

**ILANI** inatolewa kwamba, kwa mujibu wa hitaji la Sehemu za 13(g), na 69(1) ya Sheria ya Mpango wa Miji na Mpango wa Matumizi ya Ardhi, 2019 ikisomwa pamoja na Notisi ya Sheria Nambari 27 ya 2020, utayarishaji wa mpango uliotajwa hapo juu ulikamilika mnamo Februari 14, 2025.

Mpango huo wa Ustawishaji unahusu eneo lililoko ndani ya Manisipaa ya Kapsabet—Kaunti ya Nandi.

Nakala za Mpango huo wa Ustawishaji ulivyotayarishwa umehifadhiwa kwa ukaguzi na umma, bila malipo, katika Afisi za **Kamishna wa Kaunti ya Nandi** , **WAZIRI WA KAUNTI Anayesimamia Idara ya Mpango wa Miji na Matumizi ya Ardhi-Kaunti ya Nandi** na **Mkurugenzi wa Kitaifa wa Idara ya Mpango wa Miji-Orofa ya 5 Jumb la Ardhi House, Nairobi; kati ya saa mbili za asubuhi (8.00 am) na saa kumi na moja jioni (5.pm), Jumatatu hadi Ijumaa.**

Mtu yeyote ambaye angetaka kutoa maoni au pingamizi kuhusu Mpango wa Ustawishaji uliotajwa hapo juu anaweza kuziwasilisha, kwa maandishi, ili zipokelewe na Mkurugenzi wa Kitaifa wa Idara ya Mpango wa Miji, barabara ya 1st Ngong' Avenue, Jumba la Ardhi House, S.L.P. 45025-00100, Nairobi au zitumwe kwa njia ya barua pepe: ndpp@ardhi.go.ke ndani ya siku sitini (60) baada ya kuchapishwa kwa ilani hii. Na maoni au pingamizi hizo sharti ziandamanishwe na sababu zilizochangia kutolewa kwazo..

**TAREHE** Februari 25, 2025.
Dkt Peris Mang'ira, PhD, HSC
**MKURUGENZI WA KITAIFA WA IDARA YA MPANGO WA MIJI**